



NISHATI

HABARI ZA
NISHATI

News **Bulletin**

www.nishati.go.tz [Wizara ya Nishati](#) [wizara_ya_nishati_tanzania](#) [@Nishati2017](#) [Wizara ya Nishati](#)

Toleo Namba 22

Januari 1-31, 2021

Waziri na Naibu Waziri wa Nishati wafanya kikao cha kwanza na Bodi za Taasisi



Watoa
maelekezo
mahususi

Waziri wa Nishati, Mhe. Dkt Medard Kalemani (kushoto) na Naibu Waziri wa Nishati, Mhe. Stephen Byabato

**WAZIRI KALEMANI AUTAKA UONGOZI WA WIZARA YA NISHATI
KUFANYA KAZI KWA KASI, KWA UBUNIFU NA KWA USAHIHI**



**LIMEANDALIWA NA KITENGO CHA
MAWASILIANO SERIKALINI, WIZARA YA NISHATI**

Wasiliana nasi kwa simu namba +255-26-2322018 Nukushi +255-26-2320148 au
Fika Ofisi ya Mawasiliano, Mji Mpya wa Serikali Mtumba, S.L.P 2494, Dodoma

Waziri na Naibu Waziri wa Nishati wafanya kikao cha kwanza na Bodi za Taasisi



Waziri wa Nishati, Mhe. Dkt Medard Kalemani akizungumza katika kikao na Wenyeviti pamoja na Wajumbe wa Bodi za Taasisi zilizo chini ya Wizara ya Nishati. Kikao hicho kilifanyika katika Ofisi za Wizara ya Nishati, Mtumba jijini Dodoma. Kushoto kwake ni Naibu Waziri wa Nishati, Mhe. Stephen Byabato.

Na Teresia Mhagama,
Dodoma

Waziri wa Nishati, Mhe. Dkt Medard Kalemani pamoja na Naibu Waziri wa Nishati, Mhe. Stephen Byabato wamefanya kikao kazi cha kwanza na Bodi za Taasisi zilizo chini ya Wizara ya Nishati na kutoa maelekezo mbalimbali ikiwemo kutoa ukomo wa ukamilishaji wa miradi mbalimbali ya nishati nchini.

Kikao hicho



Naibu Waziri wa Nishati, Mhe. Stephen Byabato, akizungumza katika kikao na Wenyeviti pamoja na Wajumbe wa Bodi za Taasisi zilizo chini ya Wizara ya Nishati. Kikao hicho kilifanyika katika Ofisi za Wizara ya Nishati, Mtumba jijini Dodoma. Kulia kwake ni Waziri wa Nishati, Mhe. Dkt. Medard Kalemani.

kimefanyika tarehe 12 Disemba, 2020 katika Ofisi za Wizara ya Nishati, zilizopo Mtumba jijini Dodoma na kuhudhuriwa na Kaimu Katibu Mkuu, Wizara ya Nishati, Mhandisi Leonard Masanja, Wenyeviti na Wajumbe wa Bodi za Taasisi zilizo chini ya Wizara na Menejimenti ya Wizara ya Nishati na Taasisi.

Wenyeviti na Wajumbe wa Bodi hizo, wanatoka, Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO), Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC), Wakala wa Nishati Vijijini (REA), Mamlaka ya Udhhibiti wa Mkondo wa Juu wa Petroli (PURA), Kampuni ya Uendelezaji wa Jotoardhi (TGDC), Wakala wa Uagizaji Mafuta kwa Pamoja (PBPA) na Mamlaka ya Udhhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA).

Waziri wa Nishati amesema kuwa, ili nchi iweze kuwa na nishati ya kutosha, ni muhimu miradi mbalimbali ya nishati ikiwemo ya umeme na gesi ikakamilika kwa wakati na ameagiza mradi wa umeme wa Julius Nyerere (JNHPP) utakaozalisha megawati 2115 ukamilike ifikapo tarehe 14 Juni 2022.

Aidha, amesema kuwa, maandalizi ya mradi wa umeme wa Ruhudji yalishaanza

INAENDELEA UK. 4



BODI YA UHARIRI

Mwenyekiti
Mhandisi Zena Said
(Katibu Mkuu)

Makamu Mwenyekiti
Mhandisi Leonard Masanja
(Naibu Katibu Mkuu)

Mhariri
Dorina G. Makaya

Waandishi
Teresia Mhagama
Zuena Msuya
Hafsa Omar

Msanifu Kurasa
Lucas Gordon

Wasiliana nasi kwa simu
namba +255-26-2322018
Nukushi: +255-26-2320148
au

Fika Ofisi ya Mawasiliano
Mitumba Dodoma,
S.L.P 2494, Dodoma

 www.nishati.go.tz

 [Wizara ya Nishati](#)

 [@Nishati2017](#)

 [wizara_ya_nishati_tanzania](#)

 [Wizara ya Nishati](#)

Kikao cha Waziri na Naibu Waziri wa Nishati na Bodi za Taasisi chatoa muelekeo uendelezaji Sekta ya Nishati nchini

Mara baada ya Mhe. Dkt. Medard Kalemani kuapishwa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. John Pombe Magufuli kuwa Waziri wa Nishati na Mhe. Stephen Byabato kuapishwa kuwa Naibu Waziri wa Nishati, mnamo tarehe 9 Disemba, 2020 walifanya kikao cha kwanza na Wajumbe wa Bodi za Taasisi zilizo chini ya Wizara.

Kikao hicho cha Waziri wa Nishati na Naibu Waziri wa Nishati pamoja na Bodi za Taasisi zilizo chini ya Wizara ya Nishati kililenga katika kutoa maelekezo mbalimbali ikiwemo kutoa ukomo wa ukamilishaji wa miradi mbalimbali ya nishati nchini.

Maelekezo waliyoyotoa viongozi hao yanatoa muelekeo wa utekelezaji wa miradi mbalimbali ya nishati nchini ili kuweza kuwa na nishati ya kutosha.

Baadhi ya maelekezo waliyoyotoa viongozi hao ni pamoja na mradi wa umeme wa Julius Nyerere (JNHPP) utakaozalisha megawati 2115 ukamilike ipkapo tarehe 14 Juni 2022.

Aidha, kwa kuwa, maandalizi ya mradi wa umeme wa Ruhudji yalishaanza, walitoa agizo kuwa, manunuzi ya mradi huo utakaozalisha umeme wa kiasi cha megawati 358, yakamilike ipkapo mwezi Juni 2021.

Pia katika kikao hicho iliagizwa kuwa, mradi wa umeme wa Rumakali utakaozalisha megawati 222, uanze kwani lengo la Serikali ni kuwa na umeme wa kutosha utakaotosheleza mahitaji.

Vilevile, kuhusu mradi wa

umeme wa Kinyerezi I Extension utakaozalisha umeme wa kiasi cha megawati 185, waliagiza kuwa, ukamilike ndani ya miezi Sita kutoka sasa.

Kuhusu mradi wa usambazaji umeme vijijini, iliagizwa kuwa, vijiji vyote ambavyo bado havijasambaziwa umeme, viwe vimeunganishwa na umeme ipkapo mwezi Desemba mwaka 2022.

Aidha, miradi ya ujenzi wa miundombinu ya kusaPrisha umeme kutoka Tabora hadi Kidahwe-Kigoma na ule wa Ipole mkoani Tabora hadi Katavi, yote ikamilike ndani ya miezi minane ili mikoa yote Tanzania Bara iwe imeunganishwa na gridi ya Taifa.

Kuhusu Mafuta na Gesi Asilia, iliagizwa kuwa, TPDC wajikite katika masuala ya uchimbaji baada ya kufanya taPti nyingi kwani gesi inahitajika kwa matumizi mbalimbali ikiwemo majumbani na pia wananchi wanatarajia kuona mafuta hivyo ndani ya miezi Saba kuwe na dalili za uchimbaji wa mafuta.

Vilevile, kuhusu ujenzi wa vituo vidogo vya mafuta hadi vijijini ili kuwaondolea adha wananchi ya kusaPri umbali mrefu kufuata huduma hiyo, iliagizwa kuwa, EWURA itoe taarifa ya utekelezaji wa agizo hilo ndani ya miezi mitatu.

Maelekezo hayo muhimu waliyoyotoa viongozi wa Wizara, hakika yanatoa muelekeo wa nini kinapaswa kufanyika ili kuweza kuwa na nishati ya kutosha nchini ambayo itawezesha shughuli za kiuchumi na kijamii kufanyika kwa ufanisi hasa katika kipindi hiki ambacho Tanzania ipo katika Uchumi wa Kati.

Waziri na Naibu Waziri wa Nishati wafanya kikao cha kwanza na Bodi za Taasisi

INATOKA UK. 2

hivyo alitoa agizo kuwa, manunuzi ya mradi huo utakaozalisha umeme wa kiasi cha megawati 358, yakamilike ifikapo mwezi Juni 2021 kwani kipaumbele ni kuwa na umeme wa kutosha nchini.

Pia ameagiza kuwa, mradi wa umeme wa Rumakali utakaozalisha megawati 222, uanze kwani lengo la Serikali ni kuwa na umeme wa kutosha utakaotosheleza mahitaji.



Baadhi ya Wajumbe wa Menejimenti ya Wizara ya Nishati wakiwa katika kikao cha Waziri wa Nishati, Mhe. Dkt. Medard Kalemani, Naibu Waziri wa Nishati, Mhe. Stephen Byabato na Wenyeviti pamoja na Wajumbe wa Bodi za Taasisi zilizo chini ya Wizara ya Nishati. Kikao hicho kilifanyika katika Ofisi za Wizara ya Nishati, Mtumba jijini Dodoma.



Baadhi ya Wenyeviti pamoja na Wajumbe wa Bodi za Taasisi zilizo chini ya Wizara ya Nishati wakiwa katika kikao na Waziri wa Nishati, Mhe. Dkt. Medard Kalemani pamoja na Naibu Waziri wa Nishati, Mhe. Stephen Byabato. Kikao kilifanyika katika Ofisi za Wizara ya Nishati, Mtumba jijini Dodoma.

ya umeme.

Dkt. Kalemani pia ameagiza kuwa, miradi ya ujenzi wa miundombinu ya kusafirisha umeme kutoka Tabora hadi Kidahwe-Kigoma na ule wa Ipole mkoani Tabora hadi Katavi, yote ikamilike ndani ya miezi minane ili mikoa yote Tanzania Bara iwe imeunganishwa na gridi ya Taifa.

Suala la wateja takribani 16,000 ambao wameshalipia huduma ya umeme na bado hawajaunganishwa, Waziri Kalemani ameagiza kuwa, wawe wameunganishwa na huduma hiyo ndani ya miezi minne.

Aidha, ameagiza kuwa ndani ya miezi sita kuanzia sasa, Ofisi za TANESCO zinapaswa kuwepo kwenye majengo ya Shirika badala ya kupanga kwenye majengo ya watu binafsi ili kuweza kuokoa fedha za Serikali.

Vilevile kwa wateja wanaodaiwa na TANESCO, Dkt. Kalemani ameagiza kuwa, wote wakatiwe umeme, iwe Taasisi za Umma au binafsi kwani zinahitajika fedha za kujenga miradi mbalimbali ya umeme.

Waziri wa Nishati pia ameziagiza Ofisi za TANESCO katika wilaya zote kuwa na stoo ya kuhifadhi vifaa vya umeme kama vile

Vilevile, kuhusu mradi wa umeme wa Kinyerezi I Extension utakaozalisha umeme wa kiasi cha megawati 185, ameagiza kuwa, ukamilike ndani ya miezi Sita kutoka sasa.

Akizungumzia kuhusu mradi wa usambazaji umeme vijijini, Waziri Kalemani ameagiza kuwa, vijiji 2288 ambavyo havijasambaziwa umeme, viwe vimeunganishwa na umeme ifikapo mwezi Desemba mwaka 2022 ambapo mpaka sasa Vijiji 9980 tayari vimesambaziwa nishati

Waziri na Naibu Waziri wa Nishati wafanya kikao cha kwanza na Bodi za Taasisi

INATOKA UK. 4

transfoma ili kuwa na utatuzi wa haraka pale inapotokea changamoto ya vifaa vya umeme kuharibika na kukosesha wananchi huduma ya umeme.

Kuhusu Mafuta na Gesi Asilia, Waziri Kalemani amesema kuwa, TPDC wajikite katika masuala ya uchimbaji baada ya kufanya tafiti nyingi kwani gesi inahitajika kwa matumizi mbalimbali ikiwemo

majumbani na pia wananchi wanatarajia kuona mafuta hivyo ndani ya miezi Saba kuwe na dalili za uchimbaji wa mafuta.

Akizungumzia kuhusu ujenzi wa vituo vidogo vya mafuta hadi vijijini ili kuwaondolea adha wananchi ya kusafiri umbali mrefu kufuata huduma hiyo, Dkt. Kalemani ameiagiza EWURA kutoa taarifa ya utekelezaji wa agizo hilo ndani ya miezi mitatu.

Kwa upande wake Naibu Waziri wa

Nishati, Mhe. Stephen Byabato alimshukuru Waziri wa Nishati kwa maelekezo yake na kueleza kuwa yupo tayari kuyatekeleza kwa kasi, ubunifu na usahihi kwa kushirikiana na watendaji wa Wizara na Taasisi.

Kuhusu kuanzisha, kuendeleza na kumalizia miradi ya uzalishaji, usafirishaji na usambazaji umeme kwenye maeneo ya mijini na vijijini amesema kuwa atasimamia utekelezaji wa suala hilo.

Aidha, suala la umeme kukatwa kwa wateja wanaodaiwa na TANESCO, amesisitiza kuwa, agizo hilo la Waziri wa Nishati, lifanyiwe kazi kwa kuwa miradi ya umeme na Gesi ili itekelezwe, inahitaji fedha.

Kuhusu wateja takribani 16,000 waliolipia huduma ya umeme na hawajaunganishwa hadi sasa, amesisitiza kuwa, waunganishwe na huduma hiyo ndani ya miezi minne na kuongeza kuwa kuwa, wateja hao ni wale waliopita na wa sasa.

Aidha, amesema kuwa, atafuatilia suala la uwepo wa vifaa vya umeme katika ofisi za TANESCO nchini kwani uwepo wa vifaa hivyo utasaidia katika upelekaji wa huduma kwa haraka kwa wananchi.

Vilevile, amesema kuwa, umeme utaendelea kusambazwa katika visiwa mbalimbali nchini kwa gharama stahiki.

Kikao cha Waziri wa Nishati na Naibu Waziri wa Nishati pamoja na Bodi za Taasisi zilizo chini ya Wizara ya Nishati ni cha kwanza kufanyika mara baada ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. John Pombe Magufuli kuwaapisha kushika nyadhifa hizo tarehe 9 Disemba, 2020.



Kaimu Katibu Mkuu, Wizara ya Nishati, Mhandisi Leonard Masanja (kulia), Mkurugenzi wa Utawala na Rasilimali Watu, Wizara ya Nishati, Raphael Nombo (wa pili kutoka kulia), Kamishna wa Petroli na Gesi, Adam Zuberi (wa pili kutoka kushoto) na Mkurugenzi Mtendaji wa TANESCO, Dkt. Tito Mwinuka wakiwa katika kikao cha Waziri wa Nishati, Mhe. Dkt. Medard Kalemani, Naibu Waziri wa Nishati, Mhe. Stephen Byabato na Wenyeviti pamoja na Wajumbe wa Bodi za Taasisi zilizo chini ya Wizara ya Nishati. Kikao hicho kilifanyika katika Ofisi za Wizara ya Nishati, Mtumba jijini Dodoma.

WAZIRI KALEMANI AUTAKA UONGOZI WA WIZARA YA NISHATI KUFANYA KAZI KWA KASI, KWA UBUNIFU NA KWA USAHIHI

Waziri wa Nishati, Mhe. Dkt. Medard

Kalemani, amewataka watumishi wa Wizara ya Nishati kufanya kazi kwa kasi, kwa ubunifu na kwa usahihi ili kuhakikisha sekta ya Nishati inaendelea kukua ili kuwezesha upatikanaji wa umeme wa kutosha na wa uhakika kwa maendeleo ya Viwanda na kuliletea Taifa maendeleo.

Waziri Kalemani ameyasema hayo Desemba 10, 2020 wakati wa kikao na wajumbe wa



Waziri wa Nishati, Mhe. Dkt. Medard Kalemani, akizungumza na Naibu Waziri wa Nishati, Mhe. Stephen Byabato, ofisini kwake katika mji wa Serikali Mtumba, jijini Dodoma kabla ya kukutana na wajumbe wa Menejimenti ya Wizara ya Nishati.

Menejimenti ya Wizara ya Nishati



Waziri wa Nishati, Mhe. Dkt. Medard Kalemani, akimsikiliza Kaimu Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati Mha. Leonard Masanja, alipokuwa akiwasilisha taarifa ya Majukumu ya Wizara ya Nishati pamoja na Taasisi zake kwa Waziri wa Nishati Mhe. Dkt. Medard Kalemani na Naibu Waziri wa Nishati Mhe. Stephen Byabato, (hayumo pichani) kwenye kikao cha Menejimenti ya Wizara kilichofanyika kwenye ofisi za Wizara ya Nishati zilizopo Mtumba jijini Dodoma, akisikiliza kwa umakini mkubwa, kushoto kwa Kaimu Katibu Mkuu ni Mkurugenzi wa Utawala na Rasilimaliwatu, Bw. Raphael Nombo.

kilichofanyika katika ofisi za Wizara zilizopo katika Mji wa Serikali Mtumba, jijini Dodoma.

Kikao hicho cha Waziri na wajumbe wa Menejimenti ya Wizara ya Nishati,

kilichohudhuriwa na Naibu Waziri Mhe. Stephen Byabato, kililenga kutoa maelekezo ili kuwa na utekelezaji mzuri wa malengo yaliyowekwa

INAENDELEA UK. 7



Waziri wa Nishati, Mhe. Dkt. Medard Kalemani, akiwa kwenye mkutano na wajumbe wa Menejimenti ya Wizara ya Nishati (hawapo pichani).

WAZIRI KALEMANI AUTAKA UONGOZI WA WIZARA YA NISHATI KUFANYA KAZI KWA KASI, KWA UBUNIFU NA KWA USAHIHI



Naibu Waziri wa Nishati, Mhe. Stephen Byabato, akizungumza na wajumbe wa Menejimenti ya Wizara ya Nishati katika kikao kazi kilichofanyika katika ofisi za Wizara ya Nishati zilizopo Mtumba jijini Dodoma tarehe 10 Desemba, 2020.

INATOKA UK. 6

katika Sekta ya Nishati.

Akizungumza katika kikao hicho, Dkt. Kalemani ameagiza Menejimenti ya Wizara hiyo kuhakikisha kuwa umeme wa uhakika na wa kutosha unazalishwa nchini kutoka kwenye vyanzo

vya gharama nafuu hasa maji.

Pia, ameitaka Menejimenti ya Wizara ya Nishati, kuhakikisha kuwa ujenzi wa miundombinu ya kusafirishia umeme kutoka kona zote nne unakamilika kwa wakati na kuwe na mtandao wa njia ya kusambazia



Kaimu Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati Mha. Leonard Masanja akiwasilisha taarifa ya Majukumu ya Wizara ya Nishati pamoja na Taasisi zake kwa Waziri wa Nishati Mhe. Dkt. Medard Kalemani na Naibu Waziri wa Nishati Mhe. Stephen Byabato, (hawamo pichani) katika mkutano wa Menejimenti ya Wizara ya Nishati uliofanyika leo katika ofisi za Wizara hiyo zilizopo Mtumba jijini Dodoma.

umeme kwa kona zote nne kaskazini, Kusini, Mashariki na Magharibi.

Vilevile, Waziri Kalemani, ameuagiza uongozi wa Wizara ya Nishati, kuhakikisha kuwa vijiji vyote 2884 ambavyo havijaunganishwa na umeme, ifikapo mwezi Desemba 2022, viwe

vimeunganishwa na huduma hiyo.

Naye Naibu Waziri wa Nishati, Mhe. Stephen Byabato, ameahidi kutoa ushirikiano mzuri na kufanya kazi kwa weledi katika kuhakikisha majukumu ya Wizara ya Nishati yanafanyika kwa ufanisi mkubwa.



Baadhi ya wajumbe wa Menejimenti ya Wizara ya Nishati wakifuatilia kwa umakini maelekezo ya Waziri wa Nishati, Mhe. Dkt. Medard Kalemani wakati wa kikao cha Menejimenti kilichofanyika leo katika ofisi za Wizara hiyo, zilizopo Mtumba, jijini Dodoma.

DKT KALEMANI ATAKA MAELEZO YA KUSUASUA KWA MRADI WA UMEME SINGIDA -NAMANGA

HAFSA OMAR-
ARUSHA

Waziri wa Nishati, Mhe. Dkt. Medard

Kalemani, amemtaka Meneja wa mradi wa Kusafirisha umeme wa Singida hadi Namanga pamoja na msaidizi wake kutoa maelezo ndani ya siku tatu kwanini mradi wa kusafirisha umeme wa Singida hadi Namanga unasuasua.

Waziri Kalemani ameyasema hayo, Desemba 15, 2020 wakati akizungumza na waandishi wa habari mara baada



Waziri wa Nishati, Mhe. Dkt. Medard Kalemani akizungumza na Waandishi mara baada ya kukagua ujenzi wa miuondombinu ya mradi wa kusafirisha umeme wa Singida hadi Namanga mkoani Arusha, Desemba 15, 2020.

ya kukagua ujenzi wa miuondombinu ya mradi huo Mkoani Arusha.

Dkt. Kalemani, amesema mradi huo unaogharimu Dola za Marekani Milioni 258,

ulikuwa unatarajiwa kukamilika Desemba mwaka huu, lakini hadi sasa bado ujenzi wake unasuasua.

Ameeleza kuwa, kazi mojawapo ya mradi huo ni kusambaza umeme kwenye vijiji 19 katika mikoa ya Singida, Manyara na Arusha na kubainisha kuwa kusuasua kwa mradi huo kunaweza kusababisha ucheleweshaji wa usambazaji umeme kwenye vijiji hivyo jambo ambalo halikubaliki.

"Nataka kupata maelezo ni kwanini mradi huo umesimama na kwanini wafanyakazi hawapo, hatuwezi kwenda hivi. Huu mradi tunauhitaji kwa haraka, kuna vijiji vinahitaji kupelekewa umeme, nataka ujenzi wa mradi huo ukamilike haraka ili Watanzania na baadhi ya wawekezaji wanaotarajia kutumia umeme huu waanze kutumia." Amesema Dkt. Kalemani.

Aidha, kutokana na ucheleweshaji mradi huo, Dkt. Kalemani ametoa maagizo mazito ambapo amemtaka Mkandarasi wa mradi huo kufanya kazi usiku na mchana ili kuhakikisha ndani ya miezi 3 mradi huo unakamilika.

Pia ameagiza wafanyakazi



Waziri wa Nishati, Mhe. Dkt. Medard Kalemani, akiwa pamoja na wataalam mbalimbali kutoka Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) wakikagua ujenzi wa miuondombinu ya mradi wa kusafirisha umeme wa Singida hadi Namanga mkoani Arusha, Desemba 15, 2020.

DKT KALEMANI ATAKA MAELEZO YA KUSUASUA KWA MRADI WA UMEME SINGIDA -NAMANGA

INATOKA UK. 8

waongezwe haraka iwezekanavyo ili kasi ya ujenzi wa mradi huo iongezeke. Aidha, Dkt. Kalemani ameelekeza kuwa, kwa mashine zote ambazo zinatengenezwa nje ya nchi, hatua za kuzileta nchini zianze mara moja.

Vilevile, amemtaka mkandarasi na wale wote wanaosimamia mradi huo kusitisha likizo za sikukuu ili kuhakikisha mradi huo unakamilika ndani ya miezi mitatu.

“Nataka kuanza kusikia kelele za mashine hapa, hakuna kwenda Krismasi, sitaki kusikia sababu sasa hivi mvua hakuna, suala la Covid19 hapa kwetu sio tatizo tena kwahiyo ninachotaka kuona ni kazi tu hapa.” Amesema

Amefafanua kuwa, kukamilika kwa mradi huo nchi itapata umeme mkubwa kwa ajili ya kujenga uchumi wa viwanda lakini pia, kutoa ajira kwa watu wengine wakati wa ujenzi wa mradi huo.

Ameleza kuwa, ujenzi wa mradi huo ni muhimu kwa nchi na nchi za jirani kwa kuwa mradi huo utakapokamilika utaimarisha uhusiano kati ya Tanzania na nchi za jirani na itaiwezesha Tanzania kupata mapato



Waziri wa Nishati, Mhe. Dkt. Medard Kalemani, akiwa pamoja na wataalam mbalimbali kutoka Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) wakikagua ujenzi wa miuondombinu ya mradi wa kusafirisha umeme wa Singida hadi Namanga mkoani Arusha, Desemba 15, 2020.

makubwa kwa kuuza umeme kwa nchi jirani.

Akiuelezea mradi huo, Dkt. Kalemani amesema mradi huo ulianza 2017 na ulitarajiwa kukamilika ndani ya miaka 3, lakini shughuli za ujenzi rasmi zilianza 2018 na unajengwa kwa umbali wa kilomita 510 kutoka Singida Tanzania hadi Isinya Kenya ambapo kutoka Singida hadi Namanga kwa upande wa Tanzania ni kilomita 414 na Namanga hadi Isinya kwa upande wa Kenya ni kilomita 96.

Kwa upande wake, Mhandisi wa mradi

huo Bi. Blandina Joachim amesema mkandarasi wa mradi huo ameshatumia asilimia 46 ya muda

wa ujenzi wa mradi huo na anatarajiwa kumaliza ujenzi huo ndani ya miezi 3.



Mafundi wakiendelea na shughuli mbalimbali za ujenzi wa miuondombinu ya mradi wa kusafirisha umeme wa Singida hadi Namanga mkoani Arusha, Desemba 15, 2020.

DKT. KALEMANI AWATAKA VIONGOZI WA TAASISI KUFANYA KAZI KWA KASI NA UFANISI



Waziri wa Nishati Mhe. Dkt. Medard Kalemani, akizungumza na wakuu wa taasisi zilizopo chini ya Wizara ya Nishati na menejimenti zake. (hawamo pichani) Kulia kwa Waziri Kalemani, ni Naibu Waziri wa Nishati Mhe. Stephen Byabato na kushoto kwa Waziri Kalemani ni Kaimu Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati Mha. Leonard Masanja.

Waziri wa Nishati Mhe. Dkt. Medard

Kalemani, amewataka wakuu wa Taasisi zilipo chini ya Wizara ya Nishati kuhakikisha kuwa wanafanya kazi kwa ushirikiano mkubwa, kasi kubwa, ufanisi na umakini ili kuhakikisha sekta ya Nishati inazidi kukua na kuimarika kwa maendeleo ya nchi na watu wake.

Waziri Kalemani ameyasema hayo Desemba 11, 2020 wakati akiwa kwenye kikao na Wakuu wa Taasisi na Menejimenti zake zilizopo chini

ya Wizara ya Nishati, kilichofanyika jijini Dodoma. Katika kikao hicho, aliambatana na Naibu Waziri wa Nishati, Mhe. Stephen Byabato, Kaimu Katibu Mkuu Mhandishi Leonad Masanja, Kaimu Kamishna wa Umeme na Nishati Jadidifu, Edward Ishengoma, Kamishna Msaidizi wa Umeme, Mhandisi. Innocent Luoga, Mkurugenzi wa Utawala na Rasilimaliwatu, Raphael Nombo na viongozi mbalimbali wa Wizara na Taasisi zake.

Akizungumza katika kikao hicho, Dkt.

Kalemani, amewataka viongozi wa Taasisi hizo, kuhakikisha kuwa miradi yote inayotekelezwa na Wizara hiyo inakamilika kwa wakati na kwa ubora zaidi.

Aidha, Waziri Kalemani ameuwelekeza uongozi wa TANESCO kuanzia sasa kuhakikisha kuwa, hakuna mgawo wa umeme nchini na hakutokei ukataji wa umeme kabisa na pale wanapolazimika kukata umeme kutokana na sababu za msingi, taarifa itolewe kwa wananchi na warudishiwe umeme kama ilivyoahidiwa katika taarifa ya ukataji huo wa umeme.

Amesema, hii itawezesha uzalishaji viwandani pamoja na kuwezesha

INAENDELEA UK. 11



Naibu Waziri wa Nishati Mhe. Stephen Byabato akizungumza na Wakuu wa Taasisi na Menejimenti za Taasisi zilizopo chini ya Wizara ya Nishati katika Kikao kazi cha Waziri wa Nishati na Wakuu wa Taasisi na Menejimenti za Taasisi zilizopo chini ya Wizara ya Nishati.

DKT. KALEMANI AWATAKA VIONGOZI WA TAASISI KUFANYA KAZI KWA KASI NA UFANISI

INATOKA UK. 10

kufanyika kwa shughuli mbalimbali za kiuchumi na kijamii kwa wananchi wote na hivyo kupelekea

upatikanaji wa fedha zinazochangia katika ukuaji wa pato la Taifa linalotokana na Sekta ya Nishati na hivyo kulitea Taifa maendeleo makubwa ya kiuchumi.



Washiriki wa kikao kazi cha Waziri wa Nishati na Wakuu wa Taasisi na Menejimenti za Taasisi zilizopo chini ya Wizara ya Nishati, wakifuatilia kwa makini maelekezo ya Waziri wa Nishati Dkt. Medard Kalemani (hayumo pichani) wakati wa kikao kazi hicho kilichofanyika jijini Dodoma.



Washiriki wa kikao kazi cha Waziri wa Nishati na Wakuu wa Taasisi na Menejimenti za Taasisi zilizopo chini ya Wizara ya Nishati, wakifuatilia kwa makini maelekezo ya Waziri wa Nishati Dkt. Medard Kalemani (hayumo pichani) wakati wa kikao kazi hicho kilichofanyika jijini Dodoma.



Kaimu Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati Mha. Leonard Masanja (aliyesimama) akimkaribisha Waziri wa Nishati Mhe. Dkt. Medard Kalemani wakati wa kikao kazi cha Waziri wa Nishati na Wakuu wa Taasisi na Menejimenti za Taasisi zilizopo chini ya Wizara ya Nishati, Kikao kazi hicho kimefanyika kwenye Ukumbi wa Mikutano wa PSSSF eneo la Makole, jijini Dodoma.

Kwa upande wake, Naibu Waziri wa Nishati, Mhe. Stephen Byabato, amesisitiza umuhimu wa ushirikiano katika utendaji kazi, kufanya kazi kwa weledi na kujituma na amewaagiza

Wataalam wa Habari na Mawasiliano wa Wizara ya Nishati na Taasisi zake kuhakikisha taarifa za Wizara na Taasisi zake, zinawafikia wananchi kwa usahihi na kwa wakati.



DKT. KALEMANI AFANYA ZIARA BABATI KUFUATILIA MAELEKEZO YA RAIS



Waziri wa Nishati, Mhe. Dkt. Medard Kalemani, akiwa pamoja na wataalam mbalimbali kutoka Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) wakikagua ujenzi wa miuondombinu ya mradi wa kusafirisha umeme wa Singida hadi Namanga mkoani Arusha, Desemba 15, 2020.

HAFSA OMAR-MANYARA

Waziri wa Nishati, Mhe. Dkt. Medard

Kalemani, amefanya ziara wilayani Babati kufuatilia utekelezaji wa maelekezo yaliyotolewa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. John Pombe Magufuli, na kueleza kuwa ameridhishwa na utekelezaji wa maelekezo hayo.

Katika ziara hiyo

iliyofanyika Desemba 15, 2020, Waziri Kalemani ametembelea maeneo mbalimbali wilayani humo, na kuwataka wananchi wa Wilaya hiyo, waendeleo kulipia huduma ya umeme ili waweze kuunganishwa na huduma hiyo.

Akizungumza na wananchi wa kijiji cha Maisaka A, kilichopo katika kata ya Maisaka, Dkt. Kalemani amesema, amefanya ziara hiyo ili kujiridhisha endapo maelekezo yote yaliyotolewa na Rais, Mhe. Dkt. John

Pombe Magufuli yametokeleza kama yalivyoelekezwa ikiwemo agizo la kuunganishia umeme wateja 4000 ambao walikuwa bado hawajaunganishwa na umeme.

Aidha, Dkt. Kalemani amewaeleza wananchi hao kuwa, Babati mjini hakukuwa na mradi wa REA, lakini baada ya kuona wananchi wa babati wengi wao hawana uwezo wa kulipa shilingi Laki Tatu kwa ajili ya kuunganisha umeme, ametoa maelekezo kwamba wananchi hao wa Babati waanze kulipa 27,000 kama wananchi wengine

INAENDELEA UK. 13



Wananchi wa kijiji cha Maisaka A, kilichopo katika kata ya Maisaka, Mkoani Manyara, wakimsikiliza Waziri wa Nishati, Mhe. Dkt. Medard Kalemani (hayupo pichani) wakati akiwa kwenye ziara ya kikazi mkoani humo, Desemba 15, 2020.

DKT. KALEMANI AFANYA ZIARA BABATI KUFUATILIA MAELEKEZO YA RAIS



Waziri wa Nishati, Mhe. Dkt. Medard Kalemani akizungumza na baadhi ya wafanyakazi wa Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) wa wilayani Babati ili kujionea hali halisi ya ufanisi na uwajibikaji kwa wafanyakazi wa ofisi hizo, Desemba 15, 2020.

INATOKA UK.12

wanaoishi vijijini.

“Nataka kuwaeleza sababu kwanini tulichelewa, tulichelewa kwa sababu hatukuwa kwenye mpango wa 27,000 kwa hiyo tumekuja kugundua nilipotembelea Babati Mjini na kuona kwamba wananchi wa Babati ni sawa na wananchi wengine tu na wao wanastahili umeme wa 27,000.”

Alisema Dkt. Kalemani Aidha, amemuelekeza Meneja wa TANESCO kuhakikisha kuwa anaendelea na kazi ya kuunganisha umeme

kwa wateja wote wanaohitaji hudumu hiyo kwa sababu vijiji vinazidi kukua siku hadi siku na wateja wanaongezeka.

Waziri Kalemani, ameendelea kusesitiza kuwa nguzo hazizwi na kwa wale wateja wote wanaoishia mita 30 wapelekewe nguzo bila ya malipo ambapo ameeleza Watanzania wengi wanaishi katika maeneo hayo.

“Imezoeleka kasumba ya kusema hawa wapo mita 30 na wanatakiwa kulipia nguzo na walioko ndani ya mita 30 kwa Watanzania ni wengi sana kwa hiyo watakaolipa 27,000 watakuwa wachache

kwa hiyo sogezeni hizo nguzo kwa mita 30 kwa kila Mtanzania.”

Alisema Dkt. Kalemani. Hata hivyo, Dkt. Kalemani amewaeleza wananchi hao kuwa TANESCO hawataweza kuwapelekea umeme wananchi zaidi ya 100 kwa siku moja, hivyo watu wote wanapata umeme lakini hatua kwa hatua.

Pia, amewataka wananchi wote wanaopelekewa huduma ya miundombinu ya umeme wajiunganishe na huduma hiyo ili kuokoa fedha nyingi ambazo Serikali inazitoa kwa ajili ya kuwasambazia wananchi wake

umeme.

Katika hatua nyingine, Waziri Kalemani amewataka mameneja wote wa TANESCO wawasimamie wataalam wote wanaotoa namba ya kumbukumbu ya malipo (control number) na kuhakikisha wanatoa namba hizo kwa wakati bila ya kuwachelewesha wateja ili kuepuka usumbufu mkubwa kwa wateja.

Aidha, Waziri Kalemani amewataka mameneja wote wa TANESCO kuwachukulia hatua za kinidhamu watumishi wote wanaochelewesha utoaji namba ya kumbukumbu ya malipo kwa wateja bila ya sababu za msingi.

Naye, Mkuu wa Wilaya ya Babati, Lazaro Jacob Twage ameeleza kufurahishwa kwake na juhudi zinazofanywa katika kusambaza umeme katika maeneo ya vijiji na kutekeleza agizo la Mhe. Raisi kwa haraka.

Katika ziara yake hiyo, Dkt. Kalemani pia alitembelea ofisi za TANESCO Wilaya ya Babati ili kujionea hali halisi ya ufanisi na uwajibikaji kwa wafanyakazi wa ofisi hizo.

WAZIRI NA NAIBU WAZIRI WA NISHATI WAFANYA ZIARA KWENYE MRADI WA MWALIMU NYERERE



Waziri wa Nishati, Mhe. Dkt Medard Kalemani akizungumza na waandishi wa habari mara baada ya kumaliza kukagua ujenzi mradi wa mkubwa wa kufua umeme wa maji wa Julius Nyerere(JNHPP), Desemba 14, 2020.

HAFSA OMAR-RUFIJI

Waziri wa Nishati, Mhe. Dkt Medard Kalemani na Naibu Waziri wa Nishati Mhe. Stephen Byabato wamefanya ziara kwenye ujenzi wa mradi mkubwa wa kufua umeme wa maji wa Julius Nyerere (JNHPP) kwa ajili ya kujionea utekelezaji wa mradi huo ambao utazalisha umeme wa kiasi cha megawati 2115.

Ziara hiyo ilifanyika, tarehe 14 Desemba, 2020 na kuwahusisha Naibu Katiku Mkuu wa Wizara ya Nishati, Mhandisi Leonard

Masanja, Kaimu Kamishna wa Umeme na Nishati Jadidifu Edward Ishengoma, Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi TANESCO, Dkt. Alexander Kyaruzi, Mkuu mbalimbali kutoka katika Wizara ya Nishati na Taasisi zake.

Akizungumza na waandishi wa habari mara baada kumaliza kukagua mradi huo, Waziri Kalemani amesema kuwa, Serikali imekuwa ikifuatilia kwa ukaribu utekelezaji wa mradi huo, ili kuhakikisha mradi unakamilika ndani ya muda uliopangwa na kumtaka mkandarasi

kuongeza kasi ya ujenzi katika mradi huo.

“Tunataka mradi ukamilike kwa wakati na kwa kiwango

cha juu, sio mradi unakamilika baada ya miezi miwili unaanza kuhitaji tena ukarabati kwa gharama nyingine, kwa hili hatutakubali, kwa hiyo nitoe wito kwa mkandarasi kufanya kazi kwa weledi na kiwango cha juu.” Alisema Dkt. Kalemani

Dkt. Kalemani pia ametoa agizo kuwa, amesitisha likizo za sikukuu ya Krismas na Mwaka Mpya kwa mkandarasi pamoja na msimamizi wa mradi huo, ili watumie muda huo kufanya kazi kwa kasi ili mradi ukamilike kwa wakati.

Pia, amemtaka mkandarasi wa mradi huo kuhakikisha kuwa wataalam wote ambao wanahitajika kwenye mradi huo wafike mara moja kwenye mradi

INAENDELEA UK. 15



Naibu Waziri wa Nishati Mhe. Stephen Byabato akizungumza na Waandishi wa Habari mara baada ya kumaliza kukagua ujenzi mradi wa mradi mkubwa wa kufua umeme wa maji wa Julius Nyerere(JNHPP), Desemba 14, 2020.

WAZIRI NA NAIBU WAZIRI WA NISHATI WAFANYA ZIARA KWENYE MRADI WA MWALIMU NYERERE



Naibu Katiku Mkuu wa Wizara ya Nishati, Mhandisi Leonard Masanja akizungumza na Waandishi wa Habari mara baada ya kumaliza kukagua ujenzi mradi wa mradi mkubwa wa kufua umemewa maji wa Julius Nyerere (JNHPP), Desemba 14, 2020.

Mafundi wakiendelea na shughuli za ujenzi wa katika mradi mkubwa wa kufua umeme wa maji wa Julius Nyerere (JNHPP), Desemba 14, 2020.

INATOKA UK.14

huo ili kazi zifanyike kwa haraka.

Vilevile, amemtaka mkandarasi huyo kuhakikisha anajiri waatalam wote ambao wanahitajika katika ujenzi wa mradi huo na ifikapo mwisho wa mwezi huo wawe tayari wamefika nchini kwa ajili ya ujenzi huo.

Dkt. Kalemani ameingiza kuwa, mradi wa Julius Nyerere utapeleka umeme kwenye gridi ya Taifa pamoja na kwenye miundombinu

yenye uhitaji wa umeme kwa gharama nafuu.

Pia umeme huo utapelekwa kwenye vijiji 12,268 nchi nzima pamoja na kwenye Vitongoji vyake ambavyo vinafikia 64,889.

Aidha, Dkt. kalemani ameeleza kuwa, kutokana na umeme wa maji kuzalishwa kwa gharama nafuu ukilinganisha na vyanzo vingine, inatarajiwa kuwa, kukamilika kwa mradi kutasaidia kushusha bei ya umeme kwa watumiaji.

Akitoa tathmini ya jumla ya utekelezaji wa mradi, Waziri Kalemani amesema kiujumla mradi unaendelea vizuri ambapo eneo la uchepushaji maji limekamilika kwa asilimia 100, wakati eneo la ujenzi ambapo bwawa linahitajika kujengwa umbali wa mita 1,045 pamoja na kimo cha mita 131 unaendelea vizuri.

Kwa upande wake Naibu Waziri Nishati, Mhe. Stephen Byabato, ameeleza kufarijika na kasi ya ujenzi wa mradi huo na kuahidi kusimamia maagizo ya Waziri ili kuona yote yaliyoagizwa yanatekelezwa kwa wakati, ubunifu mkubwa na kwa usahihi.

Naye, Naibu Katiku Mkuu wa Wizara ya

Nishati, Mhandisi Leonard Masanja, amesema kwamba kila mmoja katika taasisi zote zilizopo chini ya Serikali ambaye kwa njia moja au nyingine anahusika katika utekelezaji wa mradi huo analojukumu la kutekeleza wajibu wake ili mradi uende kwa kasi inayotakiwa na uweze kukamilika kwa wakati.

Katika ziara hiyo, Waziri Kalemani pia alitembelea kijiji cha Mtemle kilichopo karibu na mradi huo na kuwaahidi wananchi wa kijiji hicho kuwa Serikali itakikisha inasimamia zoezi la upatikanaji wa ajira kwa usawa, kwa wananchi wote wanoishi katika wilaya zinazopakana na mradi huo.

WAZIRI NA NAIBU WAZIRI WA NISHATI WAFANYA ZIARA KWENYE MRADI WA MWALIMU NYERERE



Waziri wa Nishati, Mhe. Dkt Medard Kalemani, Naibu Waziri wa Nishati, Mhe. Stephen Byabato na Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati, Mhandisi Leonard Masanja wakiwa pamoja na Mbunge wa Rufiji Mhe. Mohamed Mchengerwa (mwenye shati nyekundu) pamoja na wataalam mbalimbali wakikagua maeneo mbalimbali ya mradi mkubwa wa kufua umeme wa maji wa Julius Nyerere (JNHPP), Desemba 14, 2020.

KALEMANI APANIA KUWIWEKA VIJJI VYOTE NCHINI NURUNI IFIKAPO DESEMBA 2022

■ NI KATIKA KUTEKELEZA MPANGO WA SERIKALI (Mpango Kabambe wa Umeme Vijijini)

Na Dorina G Makaya,
Geita.

Waziri wa Nishati, Mhe. Dkt. Medard

Kalemani, amewataka Watumishi wa Shirika la umeme Tanzania (TANESCO) mkoa wa Geita na Wilaya zake pamoja na REA, kufanya kazi kwa kasi, kwa ubunifu na kwa usahihi ili kuhakikisha vijiji vyote nchini vimeunganishwa na umeme ifikapo mwezi Desemba mwaka 2022.

Waziri Kalemani ameyasema hayo alipokuwa akizungumza na watumishi wa TANESCO Mkoa wa Geita na Wilaya zake tarehe 19 mwezi Desemba, 2020 mkoani Geita.

“ Ni kauli mbiu ya Wizara ya Nishati, na ni kauli mbiu yangu kufanya kazi kwa kasi, kwa ubunifu na kwa usahihi na kila mtumishi wa Wizara ya Nishati na Taasisi zake anapaswa kuifahamu na kutekeleza kauli mbiu hii” Amesema Dkt. Kalemani.

Waziri Kalemani ameeleza bayana kuwa, ili kuhakikisha malengo yaliyowekwa



Waziri wa Nishati, Mhe. Dkt. Medard Kalemani akizungumza wakati wa mkutano wake na watumishi wa TANESCO Mkoa wa Geita na Wilaya zake tarehe 19 mwezi Desemba, 2020 mkoani Geita.

na Serikali yanatimia, kila mtumishi katika sekta ya Nishati, anapaswa kufanya kazi kwa ubunifu na kwa uadilifu mkubwa huku akizingatia huduma nzuri kwa wateja wakati wote wa utendaji kazi.

Waziri Kalemani amesema, ni wakati muafaka kuanzia sasa kwa watumishi wote kuzingatia utoaji wa huduma nzuri kwa wateja, huku ikizingatiwa lugha nzuri na ya ushawishi kwa wateja na kuwafanya watamani kuunganishiwa huduma ya umeme hata kwa wale wenye uwezo mdogo wa kifedha.

Amesisitiza

kuwa, kuanzia sasa ni marufuku kwa mteja kulipia nguzo wala “transformer” ili kuunganishiwa umeme, kwani vifaa hivyo ni mali ya shirika la TANESCO.

Dkt. Kalemani amehoji kuhusu wateja wote walio ndani ya mita 30 wanaopaswa kuunganishiwa umeme kwa gharama ya shilingi 27,000 na kuhoji kuwa, wananchi wa vijijini wanaoishi zaidi ya mita 30 watafikiwaje na huduma hiyo iwapo TANESCO hawatawapelekea nguzo ili na wao wawe ndani ya mita 30 na kustahili kuunganishiwa umeme

kwa gharama ya shilingi elfu 27,000.

Waziri huyo wa Nishati aliyepania kuhakikisha kuwa, vijiji vyote nchini Tanzania vinaunganishiwa huduma ya umeme ifikapo mwezi Desemba mwaka 2022, ameutaka uongozi na watumishi wote wa TANESCO, kuhakikisha wanasogeza nguzo kwa wateja ili waweze kulipia huduma ya umeme kwa shilingi 27,000.

Waziri wa Nishati, Dkt. Kalemani ameelekeza kuwa, ukiondoa maeneo ya katikati ya mji, wateja wanapaswa kusogezewa nguzo hadi mita 30 ili wananchi hao wastahili kulipia umeme wa shilingi 27,000.

Dkt. Kalemani ameeleza kushangazwa kwake na ucheleweshwaji wa wateja kuunganishiwa umeme walio ndani ya mita 30, lakini bado wanacheleweshewa kuunganishiwa umeme kwa madai kwamba hadi wasubiri wapimaji waje wapime ndio wapatiwe namba ya kulipia (control number) waweze kulipia ili wapate

KALEMANI APANIA KUWIWEKA VIJJI VYOTE NCHINI NURUNI IFIKAPO DESEMBA 2022

INATOKA UK.17

kuunganishiwa huduma ya umeme.

Dkt. Kalemani amekemea vikali ucheleweshaji huo na kuweka bayana kuwa, iwapo mteja yumo ndani ya mita 30 hakuna haja ya ucheleweshaji wa wananchi kuunganishiwa huduma ya umeme kwani iko wazi ya kuwa mteja huyo yumo ndani ya mita 30 na gharama yake ni elfu 27,000 hivyo hakuna sababu ya kumchelewesha mteja huyo kupatiwa gharama za kulipia ili apatiwe huduma hiyo.

"Ni wajibu wa TANESCO kusogeza nguzo kwa mteja mita 30 ili wateja waweze kulipia huduma ya umeme kwa shilingi

27,000/= ". Amesema Waziri Medard Kalemani.

Ukiondoa maeneo ya katikati ya mji, wateja wote walioko kwenye vijiji pamoja na mitaa, wanapaswa kusogezewa umeme hadi mita 30 ili wananchi hao wastahili kulipia umeme wa shilingi 27,000.

Akizungumzia kuhusu wateja wote waliolipia kuunganishiwa huduma ya umeme wapatao 3911 katika mkoa wa Geita na wilaya zake, lakini bado hawajaunganishiwa huduma hiyo, Waziri Kalemani ametoa maelekezo ya wateja hao kuunganishiwa umeme ndani ya mwezi mmoja kuanzia sasa na ifikapo tarehe 18 mwezi Januari wawe wamepatiwa huduma

hiyo.

Waziri Kalemani ametoa maelekezo hayo, baada ya kuhakikishiwa na Kaimu Meneja Mwandamizi, TANESCO Kanda ya Ziwa, Ciprian Onyango ya kuwa, vifaa vyote kwa ajili ya kuunganishiwa wateja umeme, vipo na pia baada ya mameneja wa wilaya za Bukombe, Mbogwe, na Nyang'wale kumhakikishia Waziri Kalemani kuwa wakipatiwa vifaa hivyo kwa wakati, watahitaji si zaidi ya mwezi mmoja kukamilisha kazi hiyo ya kuunganishiwa umeme wateja wote ambao tayari wamelipia ili kuunganishiwa huduma hiyo ya umeme.

Awali akizungumza katika mkutano huo, Meneja wa TANESCO Mkoa wa Geita Eng. Joachim Ruweta alimfahamisha Waziri Kalemani kuwa, hadi sasa vijiji ambavyo bado havijaunganishiwa huduma ya umeme katika mkoa wa Geita ni vijiji 112 tu.

Dkt. Kalemani ameulekeza uongozi wa TANESCO mkoa wa Geita kwa kushirikiana na REA, kuhakikisha kuwa, vijiji hivyo viwe vimeunganishiwa huduma ya umeme ifikapo mwezi

Desemba 2021.

Akizungumzia kuhusu suala la ucheleweshaji wa kuwafanyia wateja upimaji (survey), Waziri Kalemani amesema; "kuchelewa kuwafanyia "survey" wateja kunachangia katika kupoteza mapato kwa Serikali kwani kwa kushindwa kuwahudumia wateja mapema, kunapelekea kuchelewesha kupatikana kwa mapato yanayotokana na umeme, lakini pia wateja wakilipia umeme kutaongeza mapato kwa Serikali yanayotokana na kutumia umeme." Amesema Dkt. Kalemani.

Ili kuondoa changamoto hiyo, Waziri Kalemani amewaelekeza Mameneja wote wa TANESCO kutumia rasilimali walizonazo kuwahudumia watazania.

Amelekeza kuwa, Mpimaji (Surveyor) atakayeshindwa kutekeleza wajibu wake achukuliwe hatua za kinidhamu.

"Kote kwenye mitaa na kwenye vijiji gharama ya kuunganishiwa umeme ni shilingi 27,000 tu. Ni marufuku kwa wateja kulipia nguzo wala Transforma kwani vifaa hivyo ni mali ya



Mwakilishi wa Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati Bw. Raphael Nombo akitoa ufafanuzi wa hoja zilizotolewa, kwa Waziri wa Nishati Mhe. Dkt. Medard Kalemani (kushoto kwake) wakati wa mkutano na Watumishi wa TANESCO wa Mkoa wa Geita.

KALEMANI APANIA KUWIWEKA VIJJI VYOTE NCHINI NURUNI IFIKAPO DESEMBA 2022

INATOKA UK.18

shirika la TANESCO” amesisitiza Dkt. Kalemani.

Aidha, Waziri Kalemani, ameitaka idara inayohusika na Utoaji huduma kwa wateja (Customer care department) kuweka mikakati itakayowezesha kuwafanya wapimaji wa maeneo yanayotakiwa kuunganishwa umeme (Surveyors), Watumishi wanaotakiwa kutoa namba ya malipo (Employees responsible for provision of control numbers), na Watumishi waliojiriwa kwa mikataba ya vipindi vifupi (Short Term Employee - STE) na watumishi walioajiriwa kwa mikataba ya kuanzia miezi 6 (Temporary Employee -TE), kupata elimu ya huduma kwa wateja ili waweze kutoa huduma nzuri kwa wateja, kwa kasi, kwa ubunifu na kwa usahihi kwani wao hukutana na wateja moja kwa moja, hivyo ni vema tukajenga mahusiano mazuri na wateja, kuwapa ari ya kutamani kupatiwa na kutumia huduma ya umeme, jambo litakalopelekea kuongeza mapato kwa Serikali kutokana na Sekta ya Nishati.

Vilevile, Dkt.



Watumishi wa TANESCO Mkoa wa Geita wakiwa kwenye kikao na Waziri wa Nishati Mhe. Dkt. Medard Kalemani (hayapo pichani).

Kalemani amekemea vitendo vya rushwa au kuomba pesa yoyote kwa mteja ili apatiwe huduma ya umeme.

“Sitarajii kusikia mkiomba rushwa kwa wateja. Rushwa ni adui wa haki. Hakuna kuomba rushwa kwa wateja. Hakuna kuomba “lunch” wala chai kwa wateja wala nauli. Nitakayemsikia na kumthibitisha kufanya hivyo, huyo tutaachana nae na hatua za kinidhamu zitachukuliwa dhidi yake. Ninawasihi watumishi wenzangu, msiombe, wala kupokea rushwa. Fanyeni kazi kwa kujituma na kwa uadilifu” amesema Dkt. Kalemani.

Akizungumzia kuhusu ukusanyaji wa mapato, Waziri Medard Kalemani, amewapongeza watumishi wa TANESCO mkoa wa Geita, kwa kuongoza katika ukusanyaji wa

mapato kwa kipindi cha mwezi Julai hadi Novemba mwaka 2020 ambapo waliweza kukusanya jumla ya shilingi bilioni 8.7.

Aidha, Dkt. Kalemani ameutaka uongozi wa TANESCO kuja na sera ya kuwapa motisha wafanyakazi watakaongoza katika ukusanyaji wa mapato.

“Kila Wilaya ifunge mapato kwa kushindanishwa. Ifikapo mwisho wa mwaka watumishi watakaofanya vizuri katika kukusanya mapato. Kuhudumia wateja na kufanya kazi kwa uadilifu, wapewe zawadi” amesema Waziri Kalemani.

Waziri Kalemani amesisitiza sana juu ya umuhimu wa kila kiongozi kutambua umuhimu na mchango wa kila mtumishi katika kuiwezesha Serikali kufikia malengo yake katika Sekta ya Nishati na malengo mengine ya

Kitaifa katika ujumla wake.

“Kila mtumishi anao mchango muhimu katika kufanikisha malengo tuliyojiwekea kiutendaji. Hivyo ni muhimu kutambua na kuheshimu mchango wa kila mtumishi kuanzia yule anayefanya usafi ofisini au katika eneo la kazi, anayeandaa chai, dereva hadi kiongozi wa ngazi ya juu ili kupata mafanikio mazuri katika kazi. Amesema Dkt. Kalemani.

Mkutano huo wa siku moja uliofanyika mkoani Geita, ulilenga kuwafahamu wafanyakazi, kujua changamoto walizonazo na kutoa maelekezo ya kazi. Umewakutanisha pamoja watumishi wa TANESCO mkoa wa Geita na wilaya zake pamoja na wawakilishi wa REA.

Dkt. Kalemani aipongeza TANESCO kukamilisha ujenzi kituo cha kV 220-Dodoma



Waziri wa Nishati, Mhe. Dkt. Medard Kalemani akizungumza na watendaji wa TANESCO na Wizara ya Nishati mara baada ya kukagua sehemu ya kwanza ya kazi ya upanuzi wa kituo cha umeme cha Zuzu mkoani Dodoma. Wa Pili kulia ni Kaimu Kamishna wa Umeme na Nishati Jadidifu, Edward Ishengoma na wa Tatu kulia ni Mkurugenzi Mtendaji wa TANESCO, Tito Mwinuka.

Na Teresia Mhagama,
Dodoma

Waziri wa Nishati, Mhe. Dkt. Medard Kalemani

amelipongeza Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) kwa kukamilisha sehemu ya kwanza ya kazi ya upanuzi wa kituo cha umeme cha Zuzu ambayo imepelekea mkoa wa Dodoma kuwa na umeme wa kiasi cha megawati 248 badala ya megawati 48 zilizokuwa zikipatikana

awali kutoka kwenye kituo husika.

Waziri Kalemani ametoa pongezi hizo tarehe 23 Desemba, 2020 mara baada ya kukagua kazi ya upanuzi wa kituo hicho ambapo sehemu ya kwanza ya upanuzi inahusisha ujenzi wa kituo hicho cha umeme cha kV 220 na sehemu ya pili ya upanuzi inahusisha ujenzi wa kituo cha kV 400.

Dkt. Kalemani ameeleza kuwa, alitoa agizo kuwa mradi huo ukamilike ifikapo mwezi Desemba mwaka huu na TANESCO wamefanikiwa kukamilisha kazi husika wiki iliyopita na kukifanya kituo hicho kuwa na uwezo wa megawati 248 tofauti na hapo awali ambapo kilikuwa na uwezo wa megawati 48.

INAENDELEA UK. 21



Waziri wa Nishati, Mhe. Dkt. Medard Kalemani (katikati) akizungumza na watendaji wa TANESCO na Wizara ya Nishati mara baada ya kukagua sehemu ya kwanza ya kazi ya upanuzi wa kituo cha umeme cha Zuzu mkoani Dodoma. Wa kwanza kushoto ni Mratibu wa Mradi wa Zambia-Tanzania-Kenya, Interconnector, Mhandisi Peter Kigadye.

Dkt. Kalemani aipongeza TANESCO kukamilisha ujenzi kituo cha kV 220-Dodoma

INATOKA UK. 20

Kuhusu kazi ya ujenzi wa kituo cha umeme cha kV 400 amesema kuwa, kazi nyingi zimeshafanyika hivyo alitoa agizo kuwa, kikamilike mwanzoni mwa mwezi Machi, mwaka 2021.

"Kukamilika kwa kituo hiki kunamaanisha kuwa, Dodoma sasa hivi tuna uwezo wa megawati 248 na matumizi ni megawati 48 tu kwa sasa, hivyo tuna ziada ya megawati 200." Amesema Dkt.

Kalemani Amesema kuwa, kuwepo kwa megawati 248 kunaifanya Dodoma kuwa na umeme mwingi hivyo amewakaribisha wawekezaji wa ndani na nje ya nchi kuwekeza Dodoma kwani umeme upo wa kutosha.

Dkt. Kalemani ameongeza kuwa, kwa mkoa wa Dodoma, lengo ni kuwa na megawati 648, ambapo lengo hilo litatimia mara baada ya kukamilika kwa ujenzi wa kituo cha

umeme cha kV 400 ambacho kitakamilika mwanzoni mwa mwezi Machi mwakani.

Kutokana na uwepo wa umeme huo wa kutosha, Dkt. Kalemani ametoa agizo kwa TANESCO kutokukata umeme hasa katika msimu wa sikukuu za Krismasi na Mwaka Mpya, amesema agizo hilo la kutokata umeme ni kwa nchi nzima.

Aidha, kuhusu changamoto ya wapimaji wa maeneo yanayotakiwa kuunganishiwa umeme

(surveyors) kuchelewa kutoa huduma kwa wananchi, ametoa agizo kwa TANESCO kuwanunulia pikipiki ili kuweza kutoa huduma kwa haraka.

Vilevile, kuhusu suala la ukataji wa umeme kwa wadaiwa mbalimbali zikiwemo Taasisi za Umma na Binafsi ameeleza kuwa, wateja wote wanapaswa kulipa madeni yao kwa wakati, la sivyo watakatwa umeme.

Kwa upande wake, Mratibu wa Mradi wa Zambia-Tanzania-Kenya, Interconnector, Mhandisi Peter Kigadye, ameeleza kuwa, agizo la Waziri wa Nishati, la kukamilisha ujenzi wa kituo cha kV 400, mwanzoni mwa mwezi Machi, 2021, litakamilika ndani ya muda ulioagizwa.



Waziri wa Nishati, Mhe. Dkt. Medard Kalemani (katikati) akizungumza na Waandishi wa Habari mara baada ya kukagua sehemu ya kwanza ya kazi ya upanuzi wa kituo cha umeme cha Zuzu mkoani Dodoma. Kushoto kwa Waziri ni Mkurugenzi Mtendaji wa TANESCO, Tito Mwinuka.

Wateja waliolipia ankara za umeme waunganishiwe umeme ndani ya miezi mitatu - Dkt. Kalemani

Na Dorina G. Makaya Mwanza,

Waziri wa Nishati, Mhe. Dkt. Medard

Kalemani, amewaagiza watendaji wa Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) na Wakala wa Nishati Vijijini (REA), kuhakikisha wanawaunganishia

umeme wateja wote waliolipia ankara za umeme jijini Mwanza na maeneo ya vijijini ndani ya miezi mitatu kuanzia tarehe 30 Desemba, 2020.

Waziri Kalemani ameyasema hayo, tarehe 29 Desemba, 2020, alipokuwa akizungumza na Wafanyakazi wa Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO)

na Wakala wa Nishati Vijijini (REA) katika kikao kazi cha pamoja kilichofanyika kwenye ukumbi wa Benki Kuu jijini Mwanza.

Pamoja na agizo hilo la kuwaunganishia umeme wateja hao ndani ya miezi mitatu, Waziri Kalemani, amewaelekeza watendaji hao kuhakikisha wateja wote walioko katika

maeneo ya vijijini na kando kando ya miji, wanaunganishiwa umeme kwa gharama ya Shilingi 27,000 bila kujali umbali wa mita 30 kwani ni wajibu wa TANESCO kuwafikishia wananchi nguzo za umeme ili kuwafikia wateja hao.

"Mnataka kila mwananchi awe mita 30 ndipo muwafikishie umeme? Ni kazi yenu kupeleka nguzo hadi muwafikie wananchi hao. Nisisikie mtu anaongelea suala la mita 30." amesema Kalemani

Vilevile, Waziri Kalemani, ameitaka TANESCO kuanzisha madawati ya huduma kwa wateja ili kuhakikisha wateja wanapatiwa huduma bora na kwa wakati ili kuwaondolea adha ya kufuatilia maombi ya kuunganishiwa umeme kwenye Ofisi za TANESCO wilayani.

Amewataka watendaji wa TANESCO kuwafuata wateja mahali walipo na kuepuka kutumia lugha ya kukatisha tamaa kwa wateja ili kujenga mahusiano mazuri na wateja jambo litakalopelekea kupanua wigo wa wateja na kuongeza mapato kwa Shirika.

"Masurveyor ndio wanaolalamikiwa sana kwa kutoa lugha zinazokatisha tama, ninawasihi mbadilike kuanzia sasa, atakayebainika anatomia lugha mabaya



Waziri wa Nishati, Mhe. Dkt. Medard Kalemani akizungumza na Wafanyakazi wa TANESCO na REA Mkoa wa Mwanza na Wilaya zake katika kikao kikao kilichofanyika jijini Mwanza, 29 Desemba, 2020

Wateja waliolipia ankara za umeme waunganishiwe umeme ndani ya miezi mitatu - Dkt. Kalemani

INATOKA UK. 6

kwa mteja, huyo tutaachana naye na atachukuliwa hatua za kinidhamu. Wateja wote wahudumiwe bila kubaguliwa, tunataka wateja wote wapate umeme bila kubaguliwa." Amesema Dkt. Kalemani Aidha, Dkt. Kalemani,

amewapongeza watumishi wa TANESCO kwa utendaji mzuri na kueleza kuwa kwa zaidi ya asilimia 80 utendaji wa TANESCO ni wa Kuridhisha.

Waziri Kalemani pia ameelekeza watumishi walioajiriwa kwa muda, wanaohusika na kazi za kupimia wananchi maeneo ya kuunganisha umeme,

wanunuliwe pikipiki zitakazowawezesha kuwafikia wateja kwa urahisi.

Vilevile, Waziri Kalemani amesisitiza umuhimu wa kufanya kazi kwa kasi, ubunifu na kwa usahihi na amewataka watumishi wa TANESCO na REA kujiepusha na vitendo vya rushwa.

Akizungumza na waandishi wa habari

katika kikao kazi hicho, Naibu Waziri wa Nishati, Mhe. Stephen Byabato, amewataka watumishi wote kuzingatia maelekezo yaliyotolewa na Waziri Kalemani, na kueleza kuwa atahakikisha anasimamia na kufuatilia utekelezaji wake kwa ukamilifu.

Kikao kazi baina ya Waziri Kalemani na watumishi wa TANESCO na REA, ni kikao kazi cha pili baada ya kufanya kikao na wafanyakazi wa TANESCO Mkoa wa Geita wiki iliyopita. Lengo la vikao hivyo ni kuweka misingi ya pamoja ya utendaji kazi unaolenga kuleta matokeo chanya na ya haraka katika Sekta ya Nishati.



Naibu Waziri wa Nishati, Mhe. Stephen Byabato, akizungumza na watumishi wa TANESCO na REA Mkoa wa Mwanza na Wilaya zake katika kikao kilichofanyika jijini Mwanza, 29 Desemba, 2020



Watumishi kutoka TANESCO na REA wakiwa katika mkutano wa pamoja na Waziri wa Nishati, Mhe. Dkt. Medard Kalemani pamoja na Naibu Waziri wa Nishati, Mhe. Stephen Byabato. Mkutano ulifanyika jijini Mwanza.

WAZIRI KALEMANI AIGIZA TANESCO KUWAOMBEA AJIRA WATUMISHI WALIOAJIRIWA KWA MIKATABA YA MUDA MFUPI KWA KIPINDI KIREFU

Na Dorina G. Makaya
- Shinyanga.

Waziri wa Nishati Mhe. Dkt. Medard

Kalemani, ameliagiza Shirika la TANESCO nchi nzima, kuwaombea ajira watumishi walioajiriwa kwa vipindi vifupi na kuitumikia TANESCO kwa muda mrefu.

Waziri Kalemani ametoa agizo hilo tarehe 30 Mwezi Desemba, alipokuwa akizungumza na watumishi wa TANESCO wa Mkoa wa Shinyanga, katika kikao kazi cha kufahamiana, kusikiliza kero na kutoa maelekezo ya kazi ili kuliwezesha shirika la TANESCO



Waziri wa Nishati Mhe. Dkt. Medard Kalemani, akizungumza na watumishi wa Shirika la Umeme nchini (TANESCO) katika kikao kazi kilichofanyika mjini Shinyanga tarehe 30 Mwezi Desemba 2020.

nchini kufanya kazi kama timu moja kwa kasi kwa ubunifu na kwa usahihi ili kufikisha huduma ya umeme kote nchini na kuongeza mapato ya Serikali kutokana na Sekta ya Nishati.

Akizungumza baada ya kusikiliza Kero za Watumishi wa TANESCO mkoa wa shinyanga, Waziri Kalemani ameweka bayana kuwa, watumishi hao wanaojiriwa kwa

vipindi vifupi ndio wanaokutana na wateja moja kwa moja na kujenga taswira ya TANESCO (Visibility) kwa wateja wanaohitaji na kutumia huduma ya umeme hapa nchini.

Amesema, kufanya kazi kama kibarua kwa miaka mingi bila ya kuajiriwa kwa watumishi hao, kunapunguza na pengine kuondoa hari ya kufanya kazi watumishi hao, kuleta mianya ya rushwa na hata kutengeneza vishoka.

Dkt. Kalemani ameeleza kuwa, anaamini kuajiriwa kwa watumishi hao, kutawajengea kufanya kazi kwa uaminifu na kwa kujituma kwani

INAENDELEA UK. 25



Waziri wa Nishati, Mhe. Dkt. Medard Kalemani akizungumza na wananchi wa Kitongoji cha Nyagalata, kijiji cha Nyagalata, kata ya Lunguya, wilaya ya Kahama, Halmashauri ya Msalala mkoa wa Shinyanga. Waziri Kalemani amewaahidi wananchi hao kazi ya kuleta umeme kijijini hapo inaanza tarehe 03 January 2021 na itakuwa imekamilika ndani ya miezi miwili.



Watumishi wa TANESCO wakifuatilia maelekezo yaliyokuwa yakitolewa na Waziri wa Nishati Mhe. Dkt. Medard Kalemani wakati wa kikao kazi cha Waziri wa Nishati na Watumishi wa TANESCO mkoa wa Shinyanga kilichofanyika tarehe 30 Desemba 2020.

WAZIRI KALEMANI AIGIZA TANESCO KUWAOMBEA AJIRA WATUMISHI WALIOAJIRIWA KWA MIKATABA YA MUDA MFUPI KWA KIPINDI KIREFU

INATOKA UK. 24

watahitaji kutunza ajira zao na kuonya kuwa, mtumishi yeyote atakayebainika anaomba rushwa kutoka kwa wateja na kutumia lugha zisizofaa, huyo



Naibu Waziri wa Nishati Mhe. Stephen Byabato akizungumza na watumishi wa TANESCO wakati wa kikao kazi cha Waziri wa Nishati na Watumishi wa TANESCO mkoa wa Shinyanga kilichofanyika tarehe 30 Desemba 2020. Naibu Waziri Byabato amewataka watumishi wa TANESCO kuzingatia utekelezaji wa maelekezo ya Waziri wa Nishati kwa wakati.

atondolewa mara moja na hatua za kinidhamu kuchukuliwa dhidi yake.

Akielezea kuhusu umuhimu wa kikao kazi hicho, Waziri Kalemani amefafanua kuwa, ili kuwezesha utekelezaji mzuri wa kazi, ipo haja ya kuonana na watumishi, kufahamiana, kujionea mazingira halisi ya kazi, kusikiliza kero zao na kuzitolea ufumbuzi na kisha kutoa mwelekeo na maelekezo ya kazi kufikia malengo yaliyowekwa kwenye Sekta ya Nishati.

"Unaweza kuwa unaagiza nataka kazi hii ifanyike leo na kukamilika leo hii hii, na kumbe unayempa maelekezo hayo ni mlemavu na hana uwezo wa kwenda kwa kasi hiyo. Ukaagiza afukuzwe kwa kushindwa kutekeleza kazi husika, lakini kumbe uliyemwagiza ni mlemavu. Hivyo ni muhimu kufahamiana. Amesema Dkt. Kalemani."

Aidha, Waziri huyo wa Nishati ameiagiza TANESCO, kuwanunulia pikipiki watumishi walio katika vitengo vya upimaji kwa ajili ya kufikisha umeme kwa wateja (surveyors) ili kuwezesha utendaji kazi kwa haraka na kuwaelekeza watumishi hao



Mwakilishi wa Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati, Mha. Edson Ngabo akitoa maneno ya shukrani kufuatia maelekezo ya Waziri Kalemani na kuahidi kusimamia utekelezaji wa maelekezo hayo kwenye kikao kazi cha Waziri wa Nishati na Watumishi wa TANESCO mkoa wa Shinyanga kilichofanyika tarehe 30 Desemba 2020. Kushoto kwake, ni Kaimu Mkurugenzi wa Huduma za ufundi – REA Mha. Jones Olotu, Katibu Tawala Msaidizi Bw. Bada Chamata, Waziri wa Nishati Mhe. Dk. Medard Kalemani na Naibu Waziri wa Nishati, Mhe. Stephen Byabato.

kuzitumia pikipiki hizo kwa shughuli za kikazi. "msije mkazigeuza pikipiki hizo kuwa bodaboda! Tena mziandike SU. Nataka mfanye kazi kwa kasi, kwa ubunifu, na kwa usahihi, amesema Waziri Kalemani.

Nataka kila ofisi ya TANESCO ninayo kwenda nione kuna ongezeko la mapato, nione kuna ongezeko la wateja sugu kulipa madeni wanayodaiwa TANESCO.

Waziri Kalemani ameiagiza TANESCO na REA kuhakisha vijiji vyote nchini viwe vimeunganishwa na umeme, ifikapo Septemba 2022.

Dkt. Kalemani pia ameiagiza TANESCO

kutumia nguzo za zege kwenye maeneo korofi yenye maji (Swamp areas) ili kuepusha gharama za matengenezo zinazotokana na nguzo kuanguka mara kwa mara na wateja kukosa umeme wakati matengenezo yanapokuwa yanafanyika kurejesha umeme. Aidha, Waziri Kalemani amielekeza TANESCO nchini, kutoza gharama za uunganishwaji wa umeme kwa wateja kwenye vijiji na vitongoji kwa gharama ya shilingi 27,000 tu kwa wateja wanaotumia njia moja ya umeme isipokuwa katika maeneo ya majiji.

Waziri Kalemani, aiagiza TANESCO kupeleka transfoma kwenye Mgodi wa Busolwa na Ushirika wa Isinka ifikapo tarehe 15 Januari 2021

Waziri wa Nishati, Mhe. Dkt. Medard

Kalemani, ameitaka TANESCO kupeleka transfoma mbili zenye uwezo wa MVA 2.5 na 2.0 MVA kwenye Mgodi wa Dhahabu wa Ushirikiano kati ya Busolwa na Isinka ifikapo tarehe 15 Januari 2021.

Waziri Kalemani ametoa agizo hilo tarehe 30 Desemba 2020 alipotembelea Mgodi huo. Waziri Kalemani amesema, kupatikana kwa transfoma hizo kutawezesha kupatikana umeme wa kutosha kuendesha mitambo Mgodini hapo.

Dkt. Kalemani amefafanua kuwa, mgodi huo utakapotumia umeme huo, utawezesha kupunguza zaidi ya asilimia 70 ya gharama za uzalishaji mgodini hapo.

Waziri Kalemani ameweka bayana kuwa, anatambua kuwa tayari Mgodi ulipelekewa transfoma, kwa ajili ya shughuli za ujenzi ambayo ina uwezo mdogo kulingana na mahitaji. Aidha alieleza kuwa transfoma hizo kubwa mbili zilipaswa kuwa



Waziri wa Nishati Mhe. Medard Kalemani akiwa na Naibu Waziri wa Nishati Mhe. Stephen Byabato, aliposimama kuzungumza na wananchi kuhusu huduma ya umeme na kusikiliza kero za wananchi hao kuhusiana na huduma hiyo alipokuwa njiani kuelekea kwenye Mradi wa Mgodi wa dhahabu wa Busolwa na Ushirikiano wa Isinka tarehe 30 Desemba 2020.

Waziri Kalemani, aiagiza TANESCO kupeleka transfoma kwenye Mgodi wa Busolwa na Ushirika wa Isinka ifikapo tarehe 15 Januari 2021

INATOKA UK. 26

zimefika mgodini hapo mwishoni mwa mwezi Desemba mwaka huu na ndio sababu ya kufika kwake mgodini hapo kujionea hali halisi na kutoa maelekezo.

Awali, akitoa taarifa kuhusiana na Mgodi huo, Mkurugenzi Mtendaji wa Busolwa

Mining Limited, Bw. Baraka Ezekiel alisema, upatikanaji wa transfoma hizo umekuwa ukisuasua na ni zaidi ya mwaka sasa wamekuwa wakifuatilia upatikanaji wake bila mafanikio.

Alisema. Upatikanaji wa transfoma hizo utawezesha kukamilika kwa mradi kwa wakati.

Bw. Baraka Ezekiel amesema, Mradi huo

ukikamilika, unatarajia kutoa ajira za kudumu kwa watanania zaidi ya 300 wenye taaluma mbalimbali na utakuwa chachu ya maendeleo kwa maeneo yanayozunguka mgodi wilayani Misungwi, katika mkoa wa Mwanza na Taifa kwa ujumla.

Akizungumza kufuatia maelekezo ya Waziri Kalemani,

Naibu Waziri wa Nishati, Mhe. Stephen Byabato, amewataka watumishi wa Mgodi huo kufanya kazi kwa kasi ili kuhakikisha Mradi huo unakamilika kwa wakati na amewasisitiza TANESCO kuhakikisha wanatekeleza agizo la Waziri wa Nishati kama ilivyoelekezwa.



Waziri wa Nishati, Mhe. Dkt. Medard Kalemani, akisikiliza maelezo kutoka kwa Meneja wa Mradi wa Mgodi wa dhahabu wa Busolwa na Ushirikiano wa Isinka, Bw. Ibrahim Nayopa, alipotembelea mgodi huo uliopo Kijiji cha Buhunda, Wilaya ya Misungwi, Mkoa wa Mwanza, tarehe 30 Desemba, 2020. Kushoto kwa Meneja huyo ni Mkurugenzi Mtendaji wa Mgodi huo wa Busolwa na Ushirika wa Isinka Bw. Baraka Ezekiel



Waziri wa Nishati, Mhe. Dkt. Medard Kalemani, akizungumza na Mkurugenzi Mtendaji wa Mgodi huo wa Busolwa na Ushirika wa Isinka Bw. Baraka Ezekiel, alipotembelea Mradi wa Mgodi wa dhahabu wa Busolwa na Ushirikiano wa Isinka tarehe 30 Desemba, 2020. Kushoto, ni Naibu Waziri wa Nishati, Mhe. Stephen Byabato. Mgodi huo upo Kijiji cha Buhunda, Wilaya ya Misungwi, Mkoa wa Mwanza.

ENABLING FACTORS CHIEFLY IMPORTANT FOR REALIZATION OF LOCAL CONTENT POLICY OBJECTIVES

The local content concept in the petroleum industry can be traced back to the early 1970s when Norway and UK introduced legal requirements that demanded the use of locally available workforce and materials during exploration and production of oil and gas in the North Sea. Taking an example of the Norwegian Royal Decree of 1972, this Decree required preferential treatment to local firms whenever there was an opportunity to supply goods and services provided local firms were capable to deliver the required service timely, with competitive price and meet the desired quality. Apart from giving priority to local firms, the Norwegian government imposed protectionist policies coupled with other government interventions when its oil industry was at a nascent stage in the late 1990s before it decided to embrace an



By Ebeneza Mollel

open, market oriented economy.

Following its success in diversifying the economy, the Norwegian local content policy model has since then been thought as one of the best policies to emulate. Nevertheless, since the oil and gas industry in different countries present challenges which might be completely different from what Norwegian Industry had, the need to develop a policy that suit particular country's need is critically important. It isn't a matter of copy-pasting other countries' policies and expect them to

perfectly work in another country.

Local content policies are developed for several reasons and these reasons vary from one country to another depending on what an individual country aims to achieve as an end goal. In most cases, these reasons revolve around stimulating in-country manufacturing, maximizing in-country value through the use of local workforce and locally available materials and value addition to the economy. Generally speaking, local content policies are expected to generate economic benefits above and beyond revenues

obtained from the resource sector.

Following the bizarre fact that several resource-rich countries, especially those from developing countries, have nearly failed to capture economic gain from their resources despite large Foreign Direct Investments (FDIs) flowing into the resource sector, introduction of local content policy is considered imperative. Literally speaking, the local content policy is expected to meet the needs of the industry while leveraging industry opportunities to create linkages with the rest of the economy.

Having the local content policy in place is profoundly great but for policy objectives to be realized there needs to be key enabling factors such as primary infrastructure; sound industrial policies; human capital and local supplier development programmes; and local supplier access to finance, information and requisite technology. The sheer responsibility of putting in place enabling factors belongs to host countries. It is therefore chiefly important for host countries to continue improving enabling factors for local content policies to bring desired outcome.

JARIDA HILI LA MTANDAONI HUTOLEWA NA KITENGO CHA MAWASILIANO SERIKALINI, WIZARA YA NISHATI



Fika Ofisi ya Mawasiliano,
Mji Mpya wa Serikali Mtumba, S.L.P. 2494, Dodoma au
Wasiliana nasi kwa **simu namba** +255-26-2322018
Nukushi +255-26-2320148

-  www.nishati.go.tz
-  [Wizara ya Nishati](https://www.facebook.com/Wizara.ya.Nishati)
-  [@Nishati2017](https://twitter.com/Nishati2017)
-  [wizara_ya_nishati_tanzania](https://www.instagram.com/wizara_ya_nishati_tanzania)
-  [Wizara ya Nishati](https://www.youtube.com/Wizara.ya.Nishati)